Wapanda baisikeli !

Tumia kura yako !

www.uwaba.or.tz

Asasi ya Umma wa wapanda Baisikeli Dar Es Salaam ina malengo yafuatayo:

- kuongeza usalama barabarani kwa wapanda baisikeli (wapanda baisikeli wa kawaida, wapanda baisikeli walemavu na waendesha maguta)
- kuhamasisha baisikeli kama chombo cha usafiri mjini ambacho kina faida nyingi kwa mpanda baisikeli mwenyewe, kwa jamii na kwa mazingira – kupunguza msongamano wa magari, kutochafua hewa, kusaidia watu wote kupata usafiri wa bei nafuu na wa haraka mlango hadi mlango na kuongeza afya

Mwanzoni mwa mwaka huu asasi yetu iliandika barua kwa vyama vya siasa ili kutoa maoni kwenye ilani za uchaguzi kuhusu usalama barabarani na sera zinazohusu wapanda baisikeli.Tumezipitia na kuzisoma ilani hizi kuangalia kama maoni yetu yamezingatiwa. Hapa tumeandika muhtasari wa kila chama kinasemaje katika Ilani yao kuhusu usalama barabarani, hasa kwa wapanda baisikeli na walemavu. Tunatumaini taarifa hizi zinaweza kusaidia wapanda baisikeli kutumia kura zao kuongeza usalama barabarani na kuboresha mazingira ya wapanda baisikeli.

	Ilani ya uchaguzi inasemaje	Maoni ya UWABA
Tanzania Labour Party (TLP)		
	Uk 34 “Aidha, tunaamini kwamba nyingi ya barabara zilizojengwa,zimejengwa zaidi kwa kuangalia maslahi binafsi ya viongonzi/ watawala siyo maslahi ya wanachi kwa ujumla wake.” Uk 35 “TLP itahakikisha kwamba barabara zote zinakuwa na sehemu ya watembea kwa miguu, wapanda baisikeli, na sehemu ya walemavu ili kuepusha ajali zinazowakuta wapanda baisikeli na walemavu mara kwa mara.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema wataangalia usalama wa watembea kwa miguu, wapanda baisikeli na walemavu wakati wa kujenga barabara
Chama cha Mapinduzi (CCM)		
	Uk 92 “Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazohusiana na usafiri na kukamilisha maandalizi ya kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani pamoja na kuimarisha Karakana Kuu ya Serikali.” Uk 43 “Kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART).”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara - tumepata taarifa (nje ya ilani) kwamba mradi wa DART itakuwa na njia maalum za wapanda baisikeli na pia kwa watembea kwa miguu Morogoro Road

Wapanda baisikeli !

Tumia kura yako !

www.uwaba.or.tz

Asasi ya Umma wa wapanda Baisikeli Dar Es Salaam ina malengo yafuatayo:

- kuongeza usalama barabarani kwa wapanda baisikeli (wapanda baisikeli wa kawaida, wapanda baisikeli walemavu na waendesha maguta)
- kuhamasisha baisikeli kama chombo cha usafiri mjini ambacho kina faida nyingi kwa mpanda baisikeli mwenyewe, kwa jamii na kwa mazingira – kupunguza msongamano wa magari, kutochafua hewa, kusaidia watu wote kupata usafiri wa bei nafuu na wa haraka mlango hadi mlango na kuongeza afya

Mwanzoni mwa mwaka huu asasi yetu iliandika barua kwa vyama vya siasa ili kutoa maoni kwenye ilani za uchaguzi kuhusu usalama barabarani na sera zinazohusu wapanda baisikeli.Tumezipitia na kuzisoma ilani hizi kuangalia kama maoni yetu yamezingatiwa. Hapa tumeandika muhtasari wa kila chama kinasemaje katika Ilani yao kuhusu usalama barabarani, hasa kwa wapanda baisikeli na walemavu. Tunatumaini taarifa hizi zinaweza kusaidia wapanda baisikeli kutumia kura zao kuongeza usalama barabarani na kuboresha mazingira ya wapanda baisikeli.

	Ilani ya uchaguzi inasemaje	Maoni ya UWABA
Tanzania Labour Party (TLP)		
	Uk 34 “Aidha, tunaamini kwamba nyingi ya barabara zilizojengwa,zimejengwa zaidi kwa kuangalia maslahi binafsi ya viongonzi/ watawala siyo maslahi ya wanachi kwa ujumla wake.” Uk 35 “TLP itahakikisha kwamba barabara zote zinakuwa na sehemu ya watembea kwa miguu, wapanda baisikeli, na sehemu ya walemavu ili kuepusha ajali zinazowakuta wapanda baisikeli na walemavu mara kwa mara.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema wataangalia usalama wa watembea kwa miguu, wapanda baisikeli na walemavu wakati wa kujenga barabara
Chama cha Mapinduzi (CCM)		
	Uk 92 “Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazohusiana na usafiri na kukamilisha maandalizi ya kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani pamoja na kuimarisha Karakana Kuu ya Serikali.” Uk 43 “Kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART).”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara - tumepata taarifa (nje ya ilani) kwamba mradi wa DART itakuwa na njia maalum za wapanda baisikeli na pia kwa watembea kwa miguu Morogoro Road

Chama cha Demokrasia (CHADEMA)		
	Uk 26 “Aidha, ajali za barabarani zimeendelea kuua Watanzania wengi kila mwaka, na hakuna jitihada zinafanywa na serikali ya CCM katika kukabiliana nazo, zaidi ya kutoa salamu za rambirambi kila ajali hizo zinapotokea.” Uk 29 “Kuweka mfumo thabiti wa kudhibiti matukio ya ajali barabarani. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuhakikisha vyombo vya usafiri vinakuwa katika hali ya ubora unaotakiwa, kudhibiti utoaji holela wa leseni za udereva, kutoa adhabu kali (vifungo na faini) kwa madereva na wamiliki wa vyombo vitakavyosababisha ajali kwa uzembe. Aidha matumizi ya mikanda ya usalama kwenye magari ya abiria na binafsi litakuwa jambo la lazima. Vile vile hakuna chombo cha abiria ambacho kitaruhusiwa kubeba abiria zaidi ya uwezo wake.” Uk 35 “Kuhakikisha kuwa miundo mbinu yote muhimu ikiwemo barabara inatengenezwa na kurekebishwa ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema hatua mbali mbali watakazochukua kuongeaza usalama barabarani na kupunguza udereva mbaya - wanasema wataangalia usalama wa walemavu wakati wa kujenga barabara - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli katika ujenzi wa barabara
Civic United Front (CUF)		
	Uk 53 “Suala zima la usalama barabarani bado limedharauliwa” “Itaweka mkakati maalum wa kuzitunza barabara zilizojengwa na kuziwekea vifaa na huduma zote za kisasa zikiwemo alama na taa za barabarani.” Uk 54 “Itasimamia usafirishaji wa barabarani kuhakikisha heshima na usalama wa abiria na mizigo. Itaimarisha usalama barabarani, kwa kuweka alama kila panapostahiki na kuzitilia nguvu sheria za barabarani, hasa zile zinazohusika na uzito wa mizigo na kasi ya mwendo.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema hatua mbali mbali watakazochukua kuongeaza usalama barabarani - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara
NCCR-Mageuzi		
	Uk 22 “Itajenga mfumo mpya wa usafiri wa barabara na reli katika mijimikubwa ikianzia Dar es Salaam ili kuondoakero ya msongamano wa magari, uhaba wa usafiri na ajali zinazosababiswa na barabara mbovu na nyembamba"	- ni vizuri wanatamka ajali za barabarani - wanasema wataangalia malengo ya kupunguza ajali wakati wa kuandaa mfumo wa usafiri - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)
PO Box 90361, Manzese Sisi kwa Sisi, Dar es Salaam
0713652642 0715568512 0714623774 uwabadar@yahoo.co.uk
www.uwaba.or.tz

Chama cha Demokrasia (CHADEMA)		
	Uk 26 “Aidha, ajali za barabarani zimeendelea kuua Watanzania wengi kila mwaka, na hakuna jitihada zinafanywa na serikali ya CCM katika kukabiliana nazo, zaidi ya kutoa salamu za rambirambi kila ajali hizo zinapotokea.” Uk 29 “Kuweka mfumo thabiti wa kudhibiti matukio ya ajali barabarani. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuhakikisha vyombo vya usafiri vinakuwa katika hali ya ubora unaotakiwa, kudhibiti utoaji holela wa leseni za udereva, kutoa adhabu kali (vifungo na faini) kwa madereva na wamiliki wa vyombo vitakavyosababisha ajali kwa uzembe. Aidha matumizi ya mikanda ya usalama kwenye magari ya abiria na binafsi litakuwa jambo la lazima. Vile vile hakuna chombo cha abiria ambacho kitaruhusiwa kubeba abiria zaidi ya uwezo wake.” Uk 35 “Kuhakikisha kuwa miundo mbinu yote muhimu ikiwemo barabara inatengenezwa na kurekebishwa ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema hatua mbali mbali watakazochukua kuongeaza usalama barabarani na kupunguza udereva mbaya - wanasema wataangalia usalama wa walemavu wakati wa kujenga barabara - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli katika ujenzi wa barabara
Civic United Front (CUF)		
	Uk 53 “Suala zima la usalama barabarani bado limedharauliwa” “Itaweka mkakati maalum wa kuzitunza barabara zilizojengwa na kuziwekea vifaa na huduma zote za kisasa zikiwemo alama na taa za barabarani.” Uk 54 “Itasimamia usafirishaji wa barabarani kuhakikisha heshima na usalama wa abiria na mizigo. Itaimarisha usalama barabarani, kwa kuweka alama kila panapostahiki na kuzitilia nguvu sheria za barabarani, hasa zile zinazohusika na uzito wa mizigo na kasi ya mwendo.”	- ni vizuri wanatamka usalama barabarani - wanasema hatua mbali mbali watakazochukua kuongeaza usalama barabarani - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara
NCCR-Mageuzi		
	Uk 22 “Itajenga mfumo mpya wa usafiri wa barabara na reli katika mijimikubwa ikianzia Dar es Salaam ili kuondoakero ya msongamano wa magari, uhaba wa usafiri na ajali zinazosababiswa na barabara mbovu na nyembamba"	- ni vizuri wanatamka ajali za barabarani - wanasema wataangalia malengo ya kupunguza ajali wakati wa kuandaa mfumo wa usafiri - hawasemi chochote kuhusu mahitaji ya watembea kwa miguu wala wapanda baisikeli wala walemavu katika ujenzi wa barabara

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)
PO Box 90361, Manzese Sisi kwa Sisi, Dar es Salaam
0713652642 0715568512 0714623774 uwabadar@yahoo.co.uk
www.uwaba.or.tz